BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kuweza kukutana katika Baraza hili la Kumi, kwenye Mkutano huu wa Tatu kwa lengo la kuendesha shughuli za kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako wote kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, kwa umahiri na weledi wa hali ya juu. Nikiamini kwamba uadilifu wenu huo wa hali ya juu ndio chachu ya kuimarika kwa Demokrasia katika muhimili huu muhimu wa dola katika nchi yetu hii.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuwa Rais wa Awamu ya Nane tokea baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kweli, ni imani yetu kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kushirikiana na viongozi wenzake tukianza na Mhe. Othman Masoud Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na viongozi wengine kwa maana ya mihimili yote mitatu ya dola kwa lengo la kuleta maendeleo ya haraka kwa kushirikiana na wahisani ama wadau wa maendeleo wa ndani ya nchi na nje ya nchi, yaani *Public Private Partnership (PPP)*.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo katika kuimarisha utoaji wa huduma mbali mbali za kijamii, katika uimarishaji wa miundombinu katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa kama ambavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hiyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema, maarifa, hekima, busara na amzidishie uadilifu katika kuiongoza nchi yetu, ili iendelee kuwa katika hali bora zaidi ya amani na utulivu tuliyonayo hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mwenyekiti wao na kuiongoza Kamati hii. Vile vile, kwa muda mfupi ambao ninaiongoza Kamati hii nimepata mashirikiano mazuri kutoka kwa Wajumbe wote wa Kamati na kuniwezesha kufanikisha kazi zangu kwa wepesi, kwa hakika ni wajumbe mahiri wenye uweledi, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yahya Rashid Abdulla - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Abass Wadi - Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Haji Omar Kheri - Mjumbe
6. Mhe. Zawadi Amour Nassor - Mjumbe
7. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
8. Ndg. Mussa Issa Mussa - Katibu
9. Ndg. Azmina Hamad Khamis - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kumaliza utangulizi, sasa naomba nichukue nafasi hii adhimu kutekeleza jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kwa ajili ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ina mafungu (*votes*) mawili (2) ambalo Fungu la kwanza ni H02 na imepanga kutekeleza Programu Kuu mbili zenye Programu Ndogo tatu (3) ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni **shilingi 20,371,200,000 (Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tatu na Sabiini na Moja na Laki Mbili).** Wakati mwaka jana ilipangiwa jumla ya **shilingi 17,348,600,000 (Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Tatu na Arubaini na Nane, na Laki Sita).**

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Fungu la pili ni H03 na imepanga kutekeleza Programu Kuu Nne zenye Programu Ndogo nane (8) ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ni **shilingi 197,868,500,000 (Bilioni Mia Moja na Tisiini na Saba, Milioni Mia Nane na Sitini na Nane na Laki Tano).** Wakati mwaka jana ilipangiwa jumla ya **shilingi 100,236,100,000 (Bilioni Mia Moja, Milioni Mia Mbili na Thelathini na Sita, na Lakini Moja).**

## PROGRAMU KUU YA UCHUNGUZI NA MATIBABU

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii inatekelezwa chini ya Programu Ndogo mbili ambazo ni **SH020101 ya Huduma za Uchunguzi na SH020102 ya Huduma za Matibabu** ambapo mwaka huu imepangiwa jumla ya **shilingi 813,382,000 (Milioni Mia Nane na Kumi na Tatu, Laki Tatu na Elfu Thamanini na Mbili)**, wakati mwaka jana 2020/2021 ilipangiwa jumla ya **shilingi 1,473,177,000 (Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na Sabiini na Tatu, Laki Moja na Elfu Sabiini na Saba)**.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo, inaonesha wazi kwamba bajeti ya mwaka huu imepungua sana, hivyo itapelekea kwa baadhi ya huduma kutolewa chini ya kiwango ama kutopatikana kwa wakati husika kutokana na kupungua kwa bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha Kamati imebaini kuwa Fungu H02 Hospitali ya Mnazi Mmoja imepangiwa mapato kidogo na vyanzo vyengine

havikupangiwa fedha ikiwemo Malipo ya Huduma za Afya kwa Wagonjwa wenye BIMA, Kitengo cha Huduma za Haraka pamoja na Ukodishaji wa Mkahawa ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na sio Ukodishaji wa Majengo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuangalia kwa makini hali hiyo ya kupungua kwa bajeti katika Programu Kuu ya Uchunguzi na Matibabu, kwani hiyo ndio roho ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ama Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa ujumla, kwa maana ya kimbilio la wagonjwa wote wa Zanzibar, yaani Unguja na Pemba kwa sasa ndio Hospitali ya Rufaa.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo kuhusu suala la mapato kwa Fungu H02 Hospitali ya Mnazi Mmoja kutowekewa mapato kwa mwaka wa 2021/2022. Hivyo, hali hiyo itapelekea Mapato ya Serikali kupungua na vyanzo vipo, lakini mwaka jana au miaka iliyopita vyanzo hivyo vimepangiwa fedha kwa ajili ya Mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza tena Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kufanya marekebisho kwenye mapato hayo ya Fungu H02 Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa lengo la kuweza kuiongezea Mapato Serikali yetu.

## PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA TIBA

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Huduma za Tiba katika masuala ya bajeti ya mwaka huu imepangiwa jumla ya shilingi **122,705,936,000 (Bilioni Mia Moja na Ishirini na Mbili, Milioni Mia Saba na Tano, Laki Tisa na Elfu Thalathini na Sita)**. Wakati mwaka jana ilipangiwa jumla ya **shilingi 51,258,210,000 (Bilioni Hamsini na Moja, Milioni Mia Mbili na Hamsini na Nane, na Lakini Mbili na Elfu Kumi),** kwa lengo la kutekeleza majukumu au shughuli zilizopangwa katika Programu hii kupitia Programu Ndogo mbili.

## PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kamati inafurahishwa na hatua ya Ujenzi wa Maabara ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (*ZFDA*) iliyofikia licha ya kuwa ujenzi huo uko nje ya muda uliopangwa kukamilika

kwake, ambapo baada ya kukamilika kwa Maabara hiyo itakuwa yenye hadhi ya kitaifa na kimataifa kwa kuwa na uwezo wa kutoa huduma ndani ya nchi na hata nchi nyengine.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Kamati yangu haikupendezwa na taarifa ya kusambazwa kwa mchele ambao haukuwa na kiwango kwa ajili ya matumizi ya binaadamu, na baada ya miezi mitatu ndio ikachukuliwa hatua ya kuangamizwa kwa mchele huo, ambapo jumla ya tani 50 tu ndio zimeangamizwa kati ya tani 3000 zilizoingizwa Zanzibar. Kamati yangu ilipohoji kwa wahusika wakuu imegundua bado tani 2950 ziko madukani, ambapo tayari nyengine zimeshatumiwa kwa maana ya kuliwa na binaadamu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala hilo limejitokeza baada ya Maabara yetu ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya uzembe na kuacha kutekeleza wajibu wake wa kufanya kazi zake kwa ufanisi kama Sheria inavyoelekeza, ambapo suala hili kama inavyofahamika la uchukuwaji wa sampuli ya bidhaa ya chakula lipo katika Taasisi ya *ZFDA* kwa kushirikiana na baadhi ya taasisi nyengine zinazohusika na masuala hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya Mwaka 2006, wao ndio wenye uwezo wa Kisheria kupeleka sampuli iliyoleta mashaka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali pale inapogundulika, ambapo kwa kadhia hii Kamati imegundua umefanyika udanganyifu wa upelekaji wa sampuli ya mchele mwengine tofauti na mchele uliopo sokoni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotaka kupata taarifa kuhusiana na kadhia hii, ilielezwa kwamba agizo la kuruhusiwa kutolewa, kusambazwa pamoja kutumika kwa mchele huo usiokuwa na kiwango kwa matumizi ya binaadamu limetoka kwa Viongozi wa Juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo Kamati yangu inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kulichukulia hatua kali suala hilo la uingizwaji wa bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi na zisizo na kiwango, hali inayopelekea athari kubwa kwa wananchi ikiwemo maradhi.

## PROGRAMU KUU YA UHIFADHI WA JAMII

**Mheshimiwa Spika,** Programu nyengine ni kuhusu Uhifadhi wa Jamii, ambapo Programu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili, ambapo ni Programu Ndogo ya Ustawi wa Jamii na Programu Ndogo ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto.

## PROGRAMU NDOGO YA USTAWI WA JAMII

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inafurahishwa na utaratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea na suala la Pencheni Jamii kwa Wazee kupatiwa Pencheni kwa wale waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea na kuomba utaratibu huo uendelezwe.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hayo, wakati wa ziara za Kamati ilipata taarifa kutoka kwa Watendaji pamoja na Maafisa wa Idara ya Ustawi wa Jamii, ambapo kuna baadhi ya wazee hawafaidiki na Pencheni hiyo, ambao tayari wameshafikia umri wa miaka 70 au zaidi lakini kuna wengine wanafaidika na Pencheni hiyo ambao bado hawajafikia umri wa kupata Pencheni hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Kamati imebaini kuna upotevu mkubwa wa fedha za Serikali kupitia zoezi hili la ulipaji wa Pencheni Jamii kwa baadhi ya watu ambao wanaochukuwa fedha hizo vielelezo vyao viko tofauti na uhalisia wa umri wao na wengine wenye vibali maalum *(Power of Attorney),* kwa ajili ya kuwachukulia wazee ambao hawawezi kufika kwenye vituo vya kuchukua Pencheni hiyo wanavitumia vibaya na wengine tumegundua wazee hao wameshafariki.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo Kamati, inafurahishwa na mpango wa kufanywa kwa utafiti wa kulishughulikia suala la Pencheni Jamii kwa upana wake, kwa lengo la kuondosha changamoto zinazohusiana na utaratibu mzima wa masuala ya Pencheni Jamii kwa nchi nzima, yaani Unguja na Pemba. Aidha, Kamati inashauri katika utafiti huu kufanywa kwa umakini, ili kuyapatia ufumbuzi matatizo yote yanayohusiana na masuala ya ulipaji wa Pencheni Jamii kwa watu wasiostahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini katika ziara zake kuna changamoto katika Nyumba za Wazee Sebleni kwa baadhi ya wazee wa kike kugombaniana na kupiganiana mzee wa kiume, tatizo hilo linatokana na

kukaa kwenye jengo moja kwa maana ya mchanganyiko wazee wa kike na wa kiume, hali inayosababisha kushusha hadhi na dhamira iliyokusudiwa kwa wazee hao kuwepo katika Nyumba hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na suala hilo, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuwepo kwa utaratibu maalum wa kuwatenganisha wazee hao kwenye majengo tofauti wanayoishi katika Nyumba za Wazee Sebleni, kwani kubaki kama wanavyoishi sasa kunaweza kusababisha madhara makubwa hapo baadae.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya changamoto ya Wazee wa Sebleni Kamati pia imebaini ucheleweshwaji wa uingizwaji wa fedha za ujenzi wa ukuta wa Nyumba za Wazee Welezo. Katika hali hiyo Kamati inapata wasiwasi wa utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi huo wa ukuta wa Welezo kukamilika kwa wakati uliopangwa kwa bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto hiyo**,** Kamati inahimiza ujenzi wa mradi wa ukuta wa Nyumba za Welezo kwa ajili ya kuwaondoshea usumbufu wazee pamoja na watendaji wa Idara ya Ustawi wa Jamii, ili waishi katika hali usalama na amani katika eneo hilo na kuendelea kufurahia matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, Kamati inaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii kufuatilia kwa karibu Vituo vya Serikali pamoja na Binafsi vya Kulelea Watoto kwa lengo la kufahamu hali halisi ya uendeshaji wa vituo hivyo kuhusu fedha wanazopata kutoka kwa Wahisani pamoja na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa watoto kwenye vituo hivyo, ili watoto waishi katika mazingira salama na amani ndani ya vituo hivyo, kwani Kamati inayo taarifa kuwa kuna baadhi ya vituo hivyo vinaendeshwa kinyume na taratibu zilizopo kwa kukosa leseni pamoja na vibali vya uanzishaji wa vituo hivyo na vyengine kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA JINSIA NA WATOTO

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha Mahkama Maalum kwa ajili ya kushughulikia Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Lengo la kuanzishwa kwa Mahkama hiyo ni kumaliza kabisa suala la Vitendo vya Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto, ambavyo vimekithiri katika jamii yetu ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hilo, Kamati inatoa wito kwa jamii kuwa na mashirikiano na Mahkama hiyo, ili iweze kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni pamoja na taratibu kwa ufanisi zaidi. Hivyo, ni lazima jamii kuwa na mashirikiano katika kutoa ushahidi Mahkamani, kuacha muhali, kila mmoja kuwa mlinzi wa wanawake, watoto pamoja na jamii kwa jumla, kwa ajili ya kuweza kuishi katika hali ya amani, utulivu pamoja na usalama.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali, Kamati inasikitishwa na utaratibu wa uendeshaji wa Vituo vya Mkono kwa Mkono kwa kweli hali haiko vizuri sana kutokana na kukosekana mashirikiano ya kutosha kwa upande wa baadhi ya Maafisa wa Jeshi la Polisi utaratibu wao sio rafiki, wakati wa mwanzo wa kuzishughulikia kesi za Udhalilishaji kwenye Vituo vya Polisi, kwamba kesi hizo huwa hazipelekwi sehemu ya Dawati.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Maafisa wa Jeshi la Polisi ni wachache waliopangiwa kwenye Vituo vya Mkono kwa Mkono pamoja na kuchelewa kufika katika Vituo hivyo kutokana na kutekeleza majukumu yao ya kawaida na kutakiwa kuripoti kwanza Vituoni mwao na baadaye kwenda kwenye Vituo vya Mkono kwa Mkono ambavyo walivyopangiwa, hali inayopelekea ushughulikiaji wa kesi hizo za Udhalilishaji kuchelewa na mwisho kusababisha kupoteza ushahidi.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, kuna changamoto katika suala la uchache wa wahudumu au wasimamizi wa Vituo vya Mkono kwa Mkono (*One Stope Center*), hali ya watendaji hao kwa Unguja wako watano tu, lakini kwa Pemba yuko mmoja tu. Kwa kweli, hali hii inapelekea watendaji hao kufanya kazi katika mazingira magumu sana pamoja na kukosekana kwa ufanisi wa ufuatiliaji wa kesi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile Kamati yangu inasikitishwa kuona Mratibu wa Vituo vya Mkono kwa Mkono Pemba kubebeshwa majukumu mawili kwa wakati mmoja la Uratibu wa Vituo vyote vya Pemba na kwa upande mwengine yeye ni Msimamizi wa Kituo cha Mkono kwa Mkono Micheweni. Hali hiyo, inapelekea huduma ya Mkono kwa Mkono kukosekana kwa Wilaya ya Micheweni, pale ambapo anapokuwa anafuatilia kesi za Udhalilishaji katika Vituo vyengine.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kumcha Mratibu huyo kuendelea na kazi ya Uratibu na sio kuwa Msimamizi wa Kituo cha Micheweni na badala yake kila kituo cha Mkono kwa Mkono kupatiwa Msimamizi pamoja na waratibu, ili kuweza kupunguza mrundikano wa kesi pamoja na usimamizi usioridhisha wa kesi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kutenga bajeti maalum kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ya ununuzi wa gari kwa ajili ya shughuli za Uratibu wa Masuala ya Ufuatiliaji wa Kesi za Udhalilishaji katika Vituo vya Mkono kwa Mkono kwa upande wa Pemba, kwani Kamati imegundua Mratibu huyo hufanya kazi zake katika mazingira magumu ya ufuatiliaji pamoja na usimamizi wa kesi hizo kwa kutumia usafiri wa pikipiki kwa kuzunguka Pemba nzima, hali inapelekea maisha yake kuwa hatarini kutokana na kutekeleza majukumu hayo yakushughulikia masuala ya Udhalilishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati pia inashauri Wizara ya Afya, kupeleka Maafisa wa Ustawi wa Jamii kwenye Vituo vya Mkono kwa Mkono kwa lengo la kupunguza au kuondosha tatizo la uchache wa watendaji hao kwenye vituo hivyo. Aidha, kupeleka Madaktari wenye uwezo kutoa mafunzo kwa madaktari wapya kwa ajili ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwenye vituo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, imegundua kuwepo kwa maslahi madogo kwa watendaji hao wa Vituo vya Mkono kwa Mkono. Kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza watendaji wa Vituo vya Mkono kwa Mkono kupatiwa posho maalum pamoja na vifaa vya kutendea kazi kwa lengo la kuweza kumudu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, kutokana na idadi kubwa ya ongezeko la kesi za udhalilishaji Kamati inashauri Wizara ya Afya, kuomba Maafisa wa *ZAECA* kuwemo kwenye Vituo vya Mkono kwa Mkono, kwa lengo la kuweza kudhibiti vitendo vya rushwa, ili vitendo vya udhalilishaji viweze kuchukuliwa hatua zinazostahiki na wahalifu kuweza kutiwa hatiani na kumaliza kabisa tatizo hili kwa jamii yetu.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kukamilisha Ujenzi wa Wodi za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Kivunge. Katika hali hiyo ya kukamilika kwa ujenzi huo inatoa fursa zaidi kwa akinamama na watoto kwa Mkoa wa Kaskazini pamoja na maeneo mengine ya jirani kufaidika na huduma za mama na mtoto katika hospitali hiyo na kupunguza usumbufu kwa akinamama na watoto kufuata huduma hizo nje ya Mkoa huo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati imebaini kwamba kwenye hospitali nyingi kuna tatizo la uhaba wa vitendeakazi, kwa maana ya wafanyakazi pamoja na vifaa ikiwemo Hospitali ya Kivunge pamoja na Hospitali za Wilaya ambapo wakati wa ziara Kamati ilibaini hali hiyo kwenye hospitali hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni, Kamati haikuridhishwa na hatua za utekelezaji wa Mradi huo, kwa sababu mradi umeshachukua muda mrefu na fedha nyingi zimeshatumika tokea mwaka wa fedha 2018 hadi 2021, ambapo Mradi huu mwaka 2018/2019 uliidhinishiwa fedha na Baraza hili **shilingi 3,972,592,000 (Bilioni Tatu, Milioni Mia Tisa na Sabiini na Mbili, Laki Tano na Tisiini na Mbili Elfu).**

Pia, Mradi huu kwa mwaka 2019/2020 uliidhinishiwa tena fedha na Baraza hili **shilingi 6,500,000,000 (Bilioni Sita, na Milioni Mia Tano).** Vile vile, Mradi huu kwa mwaka 2020/2021 uliidhinishiwa tena na Baraza hili hili fedha za

utekelezaji **shilingi 6,000,000,000 (Bilioni Sita)**. Hata hivyo, mradi huu mwaka 2021/2022 umetengewa fedha **shilingi 55,000,000,000 (Bilioni Hamsini na Tano).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa kwa kusuasua kwa utekelezaji wa Mradi huo, ambapo fedha nyingi zimeidhinishwa na Baraza hili kwa vipindi tofauti bila ya kuonekana maendeleo yoyote ya mradi huo. Kamati inajiuliza kulikoni?

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuchelewa kuanza na kukamilika kwa Mradi huo hadi tunawasilisha Ripoti yetu hii ya Kamati mbele ya Baraza lako Tukufu, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kutoa maelezo ya kina kuhusu matumizi ya fedha za mradi huo zilivyotumika, kwani Kamati ilipofanya ziara katika eneo hilo haikuridhishwa na hatua waliyoikuta na fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, kuhusu Ujenzi wa Hospitali ya Chakechake nao hauko vizuri sana, licha ya fedha nyingi zimeshatumika kwenye mradi huo na bado haujakamilika na pia upo nje ya muda uliotakiwa kukamilika. Kamati, haijafurahishwa na hatua iliyofikiwa kwenye mradi huu wa maendeleo na kuchelewa kwake kunapelekea kutopatikana kwa huduma ambazo zinatarajiwa kupatikana baada ya kukamilika kwa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba Wizara za Serikali kuhakikisha kwamba kabla ya mradi haujatekelezwa kuwashirikisha Wakala wa Majengo wa Serikali (*ZBA*), kufanya tathmini kwa kushirikiana na wizara husika kuhusu mradi unaokusudiwa kutekelezwa kwa ajili ya kuepusha matatizo mbali mbali ikiwemo kutafuta mkandarasi au wakandarasi wenye uwezo pamoja na kuaminika, kwa lengo la kupata majengo yenye kiwango pamoja na kukamilika kwa miradi kwa wakati, na ile azma ya kuanzishwa kwa Wakala wa Majengo ya Serikali ifikiwe kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, katika kutekeleza kazi zake za kawaida imegundua kwamba kwa upande wa Baraza la Madaktari pamoja na Baraza la Wauguzi na Wakunga yanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Wakati Mabaraza hayo yanakusanya mapato kupitia usajili pamoja na utoaji wa leseni za Madaktari, lakini Mabaraza hayo

hayawezi kutumia fedha hizo na zote zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati, inaitaka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuweka fungu maalum katika bajeti hii, kwa ajili ya matumizi ya Mabaraza hayo, ili yaweze kujiendesha kwa ufanisi na umahiri bila ya kutegemea fedha wanazozikusanya kutokana na mapato ya leseni na vibali.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kuwaongezea maslahi ya watumishi wa Kada ya Udaktari bado kuna changamoto ya maslahi madogo katika kada hizo. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kufikiria kwa makini watumishi wa Kada ya Udaktari kuhusu maslahi yao, kwa lengo la kuweza kuwa na watumishi wengi zaidi wazawa wa Zanzibar na kuachana na kukimbia nchi yao kwa ajili ya kufuata maslahi mazuri zaidi kuliko ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuhamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi kwa lengo la kupata wataalamu wengi zaidi na waliobobea katika fani tofauti za sayansi zikiwemo za afya, uhandisi pamoja na nyenginezo kwa ajili ya kupunguza tatizo la uhaba wa wataalamu wa fani hizo za sayansi nchini mwetu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inasisitiza Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuzifanya hospitali za Wilaya kuwa ni kimbilio la wananchi wetu kwa hatua ya mwanzo kwa kupata huduma za matibabu kabla ya kuelekea Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Katika hali hiyo, ni vyema kuboreshwa kwa huduma zinazotolewa kwenye hospitali hizo za wilaya, kwa maana ya vitendeakazi ikiwemo vifaa, wafanyakazi pamoja na mambo mengine.

**Mheshimiwa Spika,** Katika suala hilo, Kamati inatoa wito kwa jamii kuwa na utaratibu wa kuzitumia Hospitali za Wilaya kwa matibabu ya mwanzo sio kukimbilia moja kwa moja Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na kupelekea msongamano kwa wagonjwa na kusababisha kuchelewa kupata huduma iliyobora pamoja na usumbufu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, inaitaka Bodi ya Hospitali Binafsi kusimamia Sheria, Kanuni pamoja na taratibu za kufungua na kufunga kwa kutoa huduma kwa Hospitali Binafsi, kwani Kamati imebaini hivi karibuni Bodi hii ilifungia baadhi ya Vituo vya Hospitali Binafsi kwa lengo la kuleta ufanisi na kuondoa changamoto za ukiukwaji wa Sheria. Jambo la kushangaza miongoni mwa wajumbe hao wa Bodi ya Hospitali Binafsi walirudi na kuvifungulia vituo hivyo kinyume na utaratibu wa Sheria kwa kupokea rushwa ya fedha na hatimaye kuviruhusu vituo hivyo kufanya kazi kinyume na matakwa ya Kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kadhia hiyo, Kamati inaiomba Wizara kupitia Bodi ya Hospitali Binafsi kuchukuliwa hatua kali za kimaadili kwa mjumbe huyo aliyefanya kadhia hiyo, ili iwe funzo kwa wajumbe wengine wenye tabia kama hizo za kuchukua maamuzi binafsi mikononi mwao bila ya kuweka mbele maslahi ya nchi na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyengine tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza.

Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliyojipangia kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

**............................**

**(Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis)**
Makamu Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**